TANGAZO LA SERIKALI NA. 74 la tarehe 20/3/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya vifungu vya 7 (1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ( USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA ZA MWAKA, 2009

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba za mwaka 2009 na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:-
"Afisa wa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi,

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba;

"Mazao" ni mazao ya kilimo yanayozalishwa katika eneo la Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au shirika lolote linalonunua mazao ndani ya Halmashauri.

"Muuzaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni au kiwanda kilichoko katika eneo la Halmashauri.

"Ushuru " maana yake ni fedha itakayolipwa na mnunuzi kama ushuru wa mazao na ni pamoja na fedha itakayolipwa na mnunuzi wa mifugo itakayonunuliwa mnadani chini ya Sheria Ndogo hizi.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kampuni au Taasisi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba yake.

Ushuru wa mazo

4.-(1) Kuanzishwa ushuru wa mazao ambao utatozwa na kukusanywa na Halmashauri kwa mazao yatakayozalishwa katika eneo la Halmashauri.

(2) ushuru huo utalipwa na mnunuzi kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Baada ya kulipa ushuru mnunuzi atawajibika kudai risiti yenye muhuri na Nembo ya Halmashauri na atawajibika kuionyesha kwa Afisa muidhiniwa Mara atakapotakiwa kufanya hivyo.

(4) Ushuru wa mazao utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utakuwa ni asilimia tano (5%) ya bei ya mauzo ya Soko. [redacted]

Uteuzi wa Wakala

5. Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, Kampuni au Taasisi kuwa wakala wa kukusanya ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi na Wakala huyo atawajibika kutekeleza masharti yote ya mtoza ushuru kama yalivyoelezwa na Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa wakala na mnunuzi

6.-(1) Ni wajibu wa kila Mnunuzi au wakala wake kutoa taarifa kwa Mkurugenzi kuhusu mazao aliyonunua.

(2) Kila Wakala atatakiwa kuwasilisha makusanyo ya ushuru kabla ya tarehe 15 ya mwezi unaofuata.

(3) Wakala yeyote ambaye hatatoa taarifa kwa Mkurugenzi au kushindwa kuwasilisha ushuru kama inavyoelekezwa katika Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

(4) Wakala atakayechelewa kuwasilisha ushuru atatozwa faini ya asilimia kumi na tano (15%) ya ushuru aliochelewa kuwasilisha.

(5) Mnunuzi atakayekwepa kulipa ushuru atawajibika kulipa ushuru aliokwepa pamoja na faini ya asilimia kumi na tano (15%) ya ushuru aliokwepa.

7 Kila Meneja, Mkurugenzi au mtu yeyote mwenye dhamana ya usimamizi wa kiwanda , shirika , chama cha ushirika anaweza kutangazwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kuwa Wakala

Leseni ya biashara

8. Kila mnunuzi au wakala atatakiwa kuwa na leseni ya biashara pamoja na kibali toka Halmashauri kitakachomruhusu kununua mazao katika eneo la Halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na. 74 (linaendelea)*

Usimamizi wa masoko

9.–(1) Masoko yote ndani ya eneo la Halmashauri yatakuwa chini ya Afisa soko ambaye atasimamia uendeshaji wa masoko hayo.

(2) ni marufuku kwa mnunuzi, muuzaji au mtu yeyote kumzuia Afisa soko au Afisa Muidhiniwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Uanzishaji wa masoko vijijini

10.–(1) Kila Kijiji ndani ya Halmashauri kitatenga eneo maalum kwa ajili ya kuuzia mazao ambapo kila muuzaji atauzia mazao yake katika eneo hilo.

(2) Asilimia 20 ya ushuru itabaki kwenye kijiji husika na asilimia 80 itakwenda Halmashauri.

Muda wa kusafirisha mazao

11.–(1) Ni marufuku kwa mnunuzi yeyote kusafirisha mazao baada ya saa 12:00 Jioni na kabla ya saa 1: 00 asubuhi.

Makosa

12.(1) Itakuwa ni kosa kwa mnunuzi yeyote :–

(a) Kusafirisha mazao aliyonunua kabla ya kulipa ushuru

(b) Kusafirisha mazao wakati wa usiku

(c) Kununua mazao bila kuwa na leseni na kibali

(d) Kukataa kuonyesha risiti aliyolipia ushuru kwa Afisa muidhiniwa

(e) Kumpa mtu, kampuni au wakala mwingine kibali chake

(2) Itakuwa ni kosa kwa muuzaji:–

(a) Kuuza mazao katika maeneo yasiyoruhusiwa.

(b) Kufanya jambo lolote litakalosababisha mnunuzi kukwepa kulipa ushuru

(3) Itakuwa ni makosa kwa wakala yeyote:–

(a) Kuchelewa kuwasilisha ushuru kwa Halmashauri

(b) Kutoa taarifa za uongo kuhusu idadi ya watu waliolipa ushuru

(c) Kuwasilisha kwa Halmashauri kiwango kidogo cha fedha kinyume na makubaliano

(d) Kumshawishi mtu yeyote, kundi la watu au taasisi wasilipe ushuru

Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo. Adhabu

JEDWALI

| NA | AINA YA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 2. | Maharage | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 3. | Ulezi | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 4, | Uwele | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 5 | Dengu/choroko | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 6. | Mihogo/udanga | 5% ya bei ya mauzo ya soko |
| 7. | Mchele | 5% ya bei ya mauzo ya soko |

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba umewekwa katika Sheria Ndogo hizi kwa mujibu wa Azimio la Halmashauri lililoketi tarehe 30/5/2008 mbele ya:–

ANTONY M.SWAGI,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba*

L.S.

SHAABANI A. NTARAMBE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba*

NAKUBALI,

Dodoma,
9/1/2009

MHE. MIZENGO K. P. PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*